# 10.5 KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**Kenya Certificate of Primary Education**

**504**

# - KISWAHILI -
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA
## Oct. 2018 Muda: Saa 1 dakika 40

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini.)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha kuchagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali 1–50 umepewa majibu **manne**. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**
**Katika kijitabu cha maswali:**

**21.** Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
   A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo.
   B. njuga, tari, kinubi, fidla.
   C. harimuni, marimba, msondo, maleba.
   D. siwa, zeze, upatu, nembo.

Jibu sahihi ni **B**.

**Katika karatasi ya majibu:**

1 [A] [B] [C] [D] 11 [A] [B] [C] [D] 21 [A] [B] [C] [D] 31 [A] [B] [C] [D] 41 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

*© 2018 The Kenya National Examinations Council*

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo **zaidi** kati ya yale uliyopewa.*

Kila kiungo cha mwili wa binadamu, __1__ __2__ mashine __3__ huwa na kazi __4__ kufanya. __5__ kiungo kimoja kitashindwa kutekeleza jukumu __6__ vingine __7__. Ni muhimu binadamu kuvitunza viungo vyake asije akaishia __8__ atakapopata shughuli zake zimekwama.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. mfano | B. zaidi | C. kama | D. sawa |
| **2.** | A. iliyo | B. ilipo | C. ilivyo | D. iliko |
| **3.** | A. – | B. , | C. ; | D. : |
| **4.** | A. inayohitajika | B. kinachohitajika | C. vinavyohitajika | D. zinazohitajika |
| **5.** | A. Angalao | B. Maadamu | C. Ingawa | D. Iwapo |
| **6.** | A. kilichotengewa | B. lililotengewa | C. zilizotengewa | D. ilivyotengewa |
| **7.** | A. vitaathiriana | B. vitaathirikia | C. vitaathiria | D. vitaathiriwa |
| **8.** | A. kujiuma kidole | B. kujifia kikondoo | C. kujitia shemere | D. kujikwaa ulimi |

Mtovu aliposimama __9__ kujibu mashtaka ya wizi wa kuku kijijini __10__ hakutarajia kwamba kosa kama lile __11__ hapo. Alikuwa amefanya mazoea kuvuna asikopanda. Hali __12__ wanakijiji waliokuwa wamechoshwa naye walimwekea mtego mkubwa wa __13__ huku __14__ kwamba pwagu hupata pwaguzi; yaani __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. kizimbani | B. ulingoni | C. jukwaani | D. kitarani |
| **10.** | A. yao | B. chao | C. mwao | D. nao |
| **11.** | A. lingemleta | B. lilimleta | C. litamleta | D. linamleta |
| **12.** | A. iliyokithiri | B. ilivyokithiri | C. ilipokithiri | D. ilikokithiri |
| **13.** | A. kumkamatia | B. kuwakamatia | C. kukamatiwa | D. kukamatika |
| **14.** | A. wameamini | B. wakiamini | C. wakaamini | D. wanaamini |

**15.** A. ukitaka kumshinda mtu mwenye maarifa zaidi tumia mikakati bora zaidi
B. ukitaka kumshinda mtu anayejua udhaifu wako tumia njia nyingi zaidi
C. ukitaka kumrekebisha mtu mwenye makosa mengi tumia njia tofauti na zake
D. ukitaka kumwadhibu mtu anayefahamu ujanja wako tumia hila kama zake

*Kutoka nambari **16** mpaka **30**, chagua jibu sahihi.*

**16.** Onyesha neno lenye silabi nane.
- A. lililoanguliwa
- B. ilifyatuka
- C. nilimvutia
- D. waliosomesheana

**17.** Chagua jibu lenye kiwakilishi kionyeshi.
- A. Wanafunzi wetu walifanya vyema lakini wale hawakufanikiwa.
- B. Kitabu hiki ni changu ilhali wenyewe wanakidai.
- C. Abiria huyo alimwonya ila yeye alizidisha mwendo.
- D. Dirisha hili lina pazia bali mengine hayana.

**18.** Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:
Mchungaji alinitunzia mbuzi huyu wangu huko kwake.
- A. Wachungaji walitutunzia mbuzi hawa wetu huko kwao.
- B. Wachungaji walinitunzia mbuzi hawa wangu huko kwake.
- C. Mchungaji alitutunzia mbuzi hawa wangu huko kwao.
- D. Mchungaji alinitunzia mbuzi hawa wetu huko kwake.

**19.** Ni sentensi ipi inayoonyesha hali ya kuagiza?
- A. Mwalimu akija atawapeleka uwanjani.
- B. Mulika alisikiliza ushauri akaokoka.
- C. Utampata ikiwa utazingatia mlivyoagana.
- D. Msaidieni kuuinua mzigo huo.

**20.** Chagua sentensi yenye maana ifuatayo:
Msanifu alimfanya Kombo kuandika barua hiyo.
- A. Msanifu aliandikiwa barua hiyo na Kombo.
- B. Msanifu alimwandikisha Kombo barua hiyo.
- C. Kombo aliandikia barua hiyo kwa Msanifu.
- D. Kombo aliandikiwa barua ya Msanifu.

**21.** Ni sentensi ipi iliyotumia kiunganishi sahihi?
- A. Sudi alipongezwa minghairi ya kupata jibu sahihi.
- B. Sehemu hizi zimestawi lau kuna raia wengi.
- C. Majani hayo yalipukutika laiti upepo haukuwa mkali.
- D. Jengo hili ndilo imara kwa mujibu wa habari aliyotoa.

**22.** Chagua sentensi yenye '**ki**' ya ngeli.
- A. Moza atakufafanulia ukifika.
- B. Kimo ndani ya kabati.
- C. Bedui alikuwa akikutafuta.
- D. Umelitatua hilo kiutuuzima.

**23.** Ni sentensi ipi iliyoakifishwa ipasavyo?
- A. Naam, "akasema," Nitakusaidia."
- B. Naam, "akasema," "nitakusaidia."
- C. "Naam," akasema, "nitakusaidia."
- D. "Naam," akasema, "Nitakusaidia."

**24.** Chagua kukanusha kwa:
Masha ameosha nguo ikatakata.
- A. Masha hajaosha nguo wala haikutakata.
- B. Masha hajaosha nguo wala haijatakata.
- C. Masha hakuosha nguo na haikutakata.
- D. Masha hakuosha nguo na haijatakata.

**25.** Bainisha usemi wa taarifa wa:
Kedi: Mwanangu, nitakupeleka kwa Nyanya kesho.
- A. Kedi alimwambia mwanawe kuwa angempeleka kwa Nyanya siku ambayo ingefuata.
- B. Kedi alimwambia mwanawe kuwa angekupeleka kwa Nyanya siku ambayo ingefuata.
- C. Kedi alimwambia mwanangu kuwa alimpeleka kwa nyanya siku hiyo.
- D. Kedi alimwambia mwanangu kuwa anakupeleka kwa Nyanya siku hiyo.

**26.** Chagua jibu sahihi.
- A. Mizani ni silabi ya mwisho katika mshororo.
- B. Tathlitha ni shairi ambalo lina beti tatu.
- C. Utao ni kipande cha pili cha mshororo wa shairi.
- D. Kina ni neno linalorudiwa katika ubeti.

**27.** Kenge ni mnyama kama mamba anayeishi nchi kavu, na ana mwili mwembamba ilhali genge ni
- A. kundi la watu ambao hufanya kazi pamoja;
- B. mahali wanapopakia mizigo kiwandani;
- C. ukingo wa majabali ulio kwenye mto;
- D. barazani mwa walinda usalama nchini.

**28.** Sentensi ifuatayo imetumia tamathali gani ya usemi?
Pumu alitii amri ya moyo wake.
- A. sitiari
- B. ishara
- C. tashhisi
- D. nahau

**29.** Ikiwa leo ni Alhamisi mtondo itakuwa
- A. Jumamosi
- B. Jumapili
- C. Jumatatu
- D. Jumanne

**30.** Chagua sentensi yenye nomino dhahania.
- A. Kinara alilizungumzia darasa.
- B. Mkulima huyu amefuga bata mzinga.
- C. Wavu huo una mashimo makubwa.
- D. Kimya kilitawala alipoingia hapo.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Bila shaka umewahi kusikia neno, 'mwalimu' likitajwa. Je, neno hili linapotajwa ni wazo gani hukujia akilini? Yumkini huenda ukaniambia kwamba mwalimu ni yule ambaye anakufundisha masomo mbalimbali darasani. Wengine huenda wakasema kwamba mwalimu ni mtu ambaye anawarithisha wengine maarifa; yawe ya darasani au nje ya darasa. Alimradi kila binadamu anaweza kutoa maana anuwai za neno hili kulingana na namna ambavyo aliathiriwa na mwalimu.

Mwalimu ni mtu yeyote mwenye ujuzi, ambaye anaupitisha ujuzi huo kwa mtu mwingine mwenye kiwango cha chini cha ujuzi. Hakika hata wewe mwanafunzi umewahi kuwa mwalimu kwa mwanafunzi mwenzako au hata mwalimu wako! Fikiria mkiwa katika darasa la kwanza au la pili, namna ulivyomfundisha mwanafunzi mwenzako namna ya kuchora maumbo mbalimbali, kuruka kamba, na hata kufunga tai. Huenda ukadhani kwamba hujawahi kumfundisha mwalimu wako lolote. Hata hivyo, kumbuka kwamba wakati unapochangia somo lolote darasani huwa unawafunza wengine, akiwemo mwalimu, kuhusu namna ya kuelezea mambo tofautitofauti katika somo hilo kwa mtindo tofauti. Pia unaweza hata kumfunza mwalimu wako maarifa mapya. Mathalani, unapopewa fursa ya kuwatambia wanafunzi wenzako ngano kutoka jamii yako unapata fursa ya kumfunza mwalimu na wanafunzi wenzako kuhusu utamaduni wa jamii yako. Kupitia ngano hizi unaweza pia kufunza namna ya utambaji.

Umuhimu wa mwalimu yeyote yule hauwezi kupuuzwa. Mwalimu humwondolea mtu ujinga kwa kumfunza maarifa mbalimbali. Wewe fikiria ulipoingia katika shule ya chekechea. Ulikuwa mgeni kabisa katika mazingira ya shule. Ulikuwa hujazoea kuishi na watu ambao si wa familia yako. Jambo la kwanza ambalo mwalimu alikufundisha lilikuwa maarifa ya kuishi na wengine. Alikufunza pia namna ya kuomba msamaha unapowakosea wenzako, pamoja na kushirikiana nao katika michezo mbalimbali bila kuumizana. Juu ya hayo, mwalimu alikufunza namna ya kutamka sauti na maneno mbalimbali. Baadaye alikufunza kuzisoma sauti, maneno na vifungu mbalimbali. Bila shaka mwalimu alikufunza pia kuandika na kuwasiliana kwa **mitindo anuwai**.

Licha ya kufunza masomo mbalimbali, mwalimu huelekeza kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinaweza kuathiri masomo ya mwanafunzi. Hushauri kuhusu namna ya kutafuta haki na kusuluhisha migogoro kwa amani. Mwalimu hukushauri kwamba hata mwenzako anapokukosea haifai kumtusi au kumwendea mwalimu kumshtaki. Njia bora ni kumwambia kwa utulivu kuwa amekukosea na kumsamehe iwapo atakuomba msamaha. Ikiwa mwenzako atashindwa kuona kosa alilokutendea, basi unaweza kumwambia mwalimu ili awaelekeze zaidi na kuwasaidia kusuluhisha tatizo lenu.

Mwalimu pia hukusaidia kutambua na kukuza vipawa vyako. Vilevile hukuelekeza kutambua udhaifu wako katika masomo na hali tofautitofauti, na kukuhimiza kutafuta mikakati ya kujiimarisha. Mathalani, ikiwa una kipawa cha ushairi, mwalimu anaweza kukitambua kupitia nyimbo mnazoimba darasani. Kwa njia hii anaweza kukusaidia kukiimarisha. Hakika wapo washairi stadi ambao walisaidiwa kufikia kiwango hiki na walimu wao. Vilevile kuna wasusi ambao wameibuka kuwa hodari kwa kusaidiwa na walimu wao wa awali katika taaluma ya ususi.

Ni dhahiri kwamba binadamu hukumbana na walimu wengi maishani. Hata hivyo ni muhimu kukumbuka kwamba japo walimu wa kawaida huwa na nia nzuri, wakakufunza ya kukufaa, kuna wengine ambao wanaweza kukufunza ya kukuhasiri. Hawa hawakufunzi kwa maneno tu, bali pia kwa vitendo. Walimu wa aina hii hukuvutia kwenye matendo yao kwa kutumia vishawishi vingi. Polepole unajikuta umenaswa kabisa; ukawa mtumwa wao. **Si ajabu kupata kwamba ukiandamana na marafiki ambao wameingilia matumizi mabaya ya vileo, utainukia kuwa mraibu sugu wa vileo hivi**. Hili hutokea pale ambapo, kwa kutaka kujitambulisha na marafiki wako, unawafuata namna bendera ifuatavyo upepo. Hivyo basi ni muhimu kuwa na msimamo thabiti hata tunapoingiliana na walimu wa aina mbalimbali, tuchuje yanayofaa kujifunza. Yale yasiyofaa tuyaambae kama ukoma.

**31.** Chagua jibu sahihi kulingana na aya ya **kwanza**.
A. Mwandishi anajua kwamba msomaji anawaza kuhusu mwalimu wake.
B. Neno, 'mwalimu' lina maana tofautitofauti kulingana na wahusika.
C. Mwalimu anapofundisha maarifa darasani watu wengi huyapitisha kwa wengine.
D. Akili inapojiwa na neno, "mwalimu", hurejelea maarifa ya nje.

**32.** Chagua jibu lifaalo kulingana na kifungu.
A. Watu wenye kiwango cha chini cha ujuzi hawajui maana ya maumbo.
B. Shughuli za mwanafunzi darasani ni njia ya kupitisha maarifa kwa wengine.
C. Mwanafunzi anapofungia tai darasani marafiki hujifunza kuifunga vyema.
D. Wakati wadogo wanaposoma wanajua kwamba hawawezi kuwafundisha wakuu wao.

**33.** Kifungu kimebainisha kwamba:
A. Utambaji ni njia ya kuonyesha sifa za jamii fulani.
B. Wanafunzi huwa na mitindo tofauti ya kutambia familia zao.
C. Mwalimu hujua utambaji anapoambiwa kuhusu ngano za wanafunzi.
D. Utamaduni wa wanafunzi huimarika wanapofundishwa utambaji darasani mwao.

**34.** Kulingana na aya ya **tatu:**
A. Maarifa anayofunzwa mwanafunzi huweza kumfanya kutompuuza mwalimu.
B. Watu wakiingia shule za chekechea hawajui familia nyingine.
C. Mwanafunzi anajua maana ya vifungu anapoingia shuleni.
D. Mwalimu anaweza kumfanya mwanafunzi kuwa mnyenyekevu.

**35.** Chagua umuhimu wa shule kulingana na aya ya **tatu**.
A. kukuza uvumilivu,, kusahau makosa;
B. kukuza utiifu, kujikinga na maumivu;
C. kukuza mazoea ya michezoni, kuimarisha hati;
D. kukuza utangamano, kustawisha mbinu za kujieleza.

**36.** Aya ya **nne** imebainisha kwamba:
A. Mwalimu anapotambua changamoto zinazotokana na masomo, alama za wanafunzi huimarika.
B. Mwanafunzi anapoelekezwa kuhusu aina za migogoro isiyofaa huwa bora masomoni.
C. Mwalimu humjengea mwanafunzi hulka ya kutafuta anachostahili bila kuwaumiza wenzake kihisia.
D. Mwanafunzi huwahimiza wenzake kujadiliana kuhusu matatizo yao kabla ya kumwarifu mwalimu.

**37.** Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa aya ya **tano**.
A. Mwanafunzi anapoimba nyimbo darasani huelewa vipawa vya wanafunzi wengine.
B. Mwalimu akimsaidia mwanafunzi yeye hupata mbinu za kuimarisha vipawa.
C. Mwalimu humwelekeza mwanfunzi kujua ubora wake katika nyanja mbalimbali.
D. Mwanafunzi anamtegemea mwalimu wa awali kufahamu namna za wasusi shuleni.

**38.** Aya ya mwisho imebainisha kwamba:
A. Maarifa ayapatayo binadamu yanaweza kutokana na vielelezo anavyoona kutoka kwenye mazingira yake.
B. Idadi kubwa ya walimu anaopata mtu huwa na ari ya kumwadilisha.
C. Watu wengi huingia kwenye mitego ya washauri kwa kutojua athari za dawa.
D. Baadhi ya wanafunzi hushirikiana na marafiki wanapojikuta wakiwa na ushawishi mdogo.

**39.** **"Si ajabu kupata kwamba ukiandamana na marafiki ambao wameingilia matumizi mabaya ya vileo, utainukia kuwa mraibu sugu wa vileo hivi."**
Chagua methali ambayo inajumuisha ujumbe wa kauli hii.
A. Mshika mbili moja humponyoka.
B. Mchezea tope haliachi kumrukia.
C. Mdharau mwiba hupata tende.
D. Mpanda ovyo hula ovyo.

**40.** Maana ya '**mitindo anuwai**' kulingana na kifungu ni mitindo:
A. ambayo haihusiani;
B. ya aina nyingi;
C. ya wasemaji tofauti;
D. ambayo haijapatikana.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Sijui kama umewahi kutambiwa hadithi kuhusu asili ya gamba la Kobe. Ama utaniambia kuwa huna nyanya wa kukusimulia kisa hiki kwa sababu, ama unaishi mjini, au nyanya yako ni mchanga, kwa hivyo hajafikia kiwango cha kuitwa nyanya? Basi msomaji, fahamu kwamba kisa cha adhabu ya Kobe kimekuwa kikisimuliwa tangu jadi.

Inasimuliwa kwamba zamani sana Kobe alikuwa anaishi katika kijiji cha Kasakine. Raia wa Kasakine walikuwa mkono wazi na wenye kupenda ushirikiano. Walifanya kazi bega kwa bega, wakajenga bwawa la maji ambalo walitumia kunyunyizia mashamba yao maji na kunyweshea mifugo wao. Ingawa Kobe alishirikiana na wanyama wenzake, alikuwa na dosari moja kuu; alikuwa mvivu. Aliona kazi ya kupalilia mashamba na kuchimba mabwawa kuwa ngumu mno. Kwa hivyo alizua mbinu za kuuficha uvivu. Kwa vile alikuwa na akili nyepesi kuliko wanyama wenzake, aliweza kupanga mikakati ya kukamilisha kazi upesi. Wanyama walimstahi kwa kipawa cha uongozi, wakamchagua kuwa kinara wao. Hapo ndipo ugoigoi wa Kobe ulipovuka mipaka.

Kila asubuhi, Kobe ndiye aliyekuwa wa kwanza kuwaamsha wenzake kwenda shambani. Hata hivyo, Kobe hakudiriki kufika shambani. Wakiwa njiani angesingizia kusikia mlio wa mnyama hatari kichakani. Hapo wenzake wangemkabidhi jukumu la kwenda kukabiliana naye. Kobe angeingia kichakani, akala shibe yake ya majani na matunda na kuwangojea wenzake hapohapo njiani wakitoka shambani adhuhuri waelekee nyumbani pamoja.

Siku moja Kobe alialikwa na kiongozi mwenzake kwenye nchi ya Kaelea iliyokuwa juu angani. Kobe alipopata barua ya mwaliko **alijishika tama** asijue la kufanya. Aliyalaani maumbile yaliyomkosesha mbawa. Hata hivyo, akili yake ilifanya kazi upesi kama kawaida, akawaambia ndege, "Ndugu zangu, nimealikwa katika nchi ya Kaelea kwenda kujifunza mengi kuhusu uongozi na jinsi wanavyoiendesha miradi yao ya kiuchumi. Rais wa huko, Bwana Kawapeni, pia ameahidi kunipa msaada wa fedha kuufadhili mradi wa kueneza umeme vijijini, Ndugu zangu, mnajua kwamba mwenzio sijiwezi, sina mbawa, nifaeni kwa jua niwafae kwa mvua." Ndege walifurahishwa sana na rai ya kiongozi wao. Waliona kwamba yeye, kinyume na Ndovu, anajali masilahi ya raia wake, na muhimu zaidi, anawathamini. Ndege wote, hata kuku na bata walimchangia Kobe mbawa.

Asubuhi na mapema Kobe na wawakilishi ishirini walipaa juu kuelekea Kaelea. Kawapeni aliwakaribisha kwa heshima kuu, akawaandalia karamu kuu. Wote walikula shibe yao. Siku iliyofuata mambo yalianza kubadilika. Kobe alivamiwa na tabia yake ya kawaida, akawa kila mara anapopewa chakula na pesa na Kawapeni, anasema, "Hiki ni chetu", na kumpa msaidizi wake wa karibu pekee, huku Kawapeni akiachwa kuamini kuwa 'chetu' ilimaanisha wote walioandamana na Kobe.

Hali iliendelea hivyo kwa muda na wiki mbili, ndege wote waliokuwa wameandamana na Kobe wakawa wamenyong'onyea kwa njaa, kwani waliweza tu kula mabaki ambayo Kobe na msaidizi wake walikuwa wamebakiza. Siku ya kurudi nyumbani ilifika, nao ndege wakawa wamesema kuwa hii ndiyo siku ya siku. Siku hiyo Kasuku aliamka mapema na kudai kwamba kabla ya kuondoka ni muhimu kutembelea kiwanda cha kuokea mikate. Wote walielekezwa huko. Kasuku alimwambia Kobe kwamba kwa vile yeye kasoma, na anaielewa lugha ya viwandani vyema, akaribie kwenye tanuri ili kuelekezwa namna linavyotumiwa.

Kobe alikaribia tanuri hilo lenye joto la ajabu bila kuwa na mwao na athari zake. Mfanyakazi wa kiwanda aliendelea kuwatolea maelezo huku Kobe anayaandika. Hata mfanyakazi alipokamilisha maelezo yake, manyoya na mbawa zote alizokuwa amechangiwa Kobe zilimomonyolewa na joto. Safari ya kurudi nyumbani nayo ilikuwa imeiva. Kobe alijaribu kuwarai ndege wamchangie tena lakini ndege walimkumbusha jinsi alivyowanyanyasa ugenini. Walianza kuteremka chini mmoja baada ya mwingine bila kumjali Kobe. Kobe aliupiga moyo wake konde akaamua **kujikuna ajipatapo**. Aliiweka mikononi yake mbele kama mwogeleaji anayepambana na maji na kujitupa chini ambako alianguka kama gunia tele. Ngozi yake laini ilikutana na majabali ikabadilika kuwa gamba.

**41.** Kulingana na aya ya **kwanza**:
- A. Wale wanaoishi mjini hawasimuliani hadithi.
- B. Hadithi ya Kobe husimuliwa na watu wazima.
- C. Utambaji wa hadithi si jambo geni katika jamii ya Kobe.
- D. Huenda msomaji amesimuliwa kuhusu chanzo cha gamba la Kobe.

**42.** Ni jibu lipi sahihi kulingana na aya ya **kwanza**?
- A. Raia wa Kasakine walikuwa wakarimu na wenye umoja.
- B. Kobe alifanikisha mipango kwa kunyunyizia mashamba maji.
- C. Kulima na kuchimba ilikuwa kazi iliyohitaji nguvu kwa wote.
- D. Kushirikiana kuliwafanya wanyama na viongozi kuheshimiana.

**43.** Aya ya **pili** imebainisha kwamba:
- A. Kobe alibuni mbinu ili kuondoa uvivu.
- B. Uvivu wa Kobe ulisababishwa na madaraka.
- C. Kobe alipata uongozi kwa sababu ya busara yake.
- D. Wepesi wa Kobe ulimfanya kutunukiwa kipawa.

**44.** Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa aya ya **tatu**.
- A. Uhodari wa kushawishi ulimfanya Kobe asijue kulima.
- B. Wanyama wenzake Kobe walichangia kuendeleza ubinafsi wake.
- C. Mazingira ya kichakani yalisababisha kutofanya kazi shambani.
- D. Jukumu la uongozi liliwafanya wengine kuendesha kazi peke yao.

**45.** Chagua tabia za Kobe kulingana na kifungu.
- A. mjanja, anayejali usalama wa wengine;
- B. mwendesha shughuli za wenzake, laghai;
- C. mwenye tamaa, asiyewaza kwa makini;
- D. mwenye huzuni, asiyeshukuru kwa mema.

**46.** Safari ya Kaelea ingeifaidi vipi nchi ya Kobe?
- A. kuonyeshwa namna ya kuelezea njia za kukuza uongozi;
- B. kufunzwa namna ya kustawisha hali ya maisha ya raia;
- C. kushauriwa kuhusu namna ya kutumia misaada ya wafadhili;
- D. kuelekezwa kuhusu namna ya kutumia umeme kuanza miradi.

**47.** Ni dhahiri kwamba ndege:
- A. walikuwa wanyonge kwa kupewa chakula mwisho;
- B. walikuwa na hamu ya kuona kiwanda;
- C. walikuwa wameamua kumrekebisha Kobe;
- D. walikuwa na matarajio ya kushauriwa na mfanyakazi.

**48.** Aya ya **mwisho** inaonyesha kuwa:
- A. Wenzake Kobe walikumbuka dhuluma nyumbani kwao.
- B. Wenzake Kobe ni wenye msimamo imara.
- C. Kobe alitumia ujuzi wake wa riadha kuteremka chini ardhini.
- D. Kobe alipata gamba kwa sababu mwili wake haukuzoea majabali.

**49.** Kauli, **alijishika tama** imetumia tamathali gani ya usemi?
- A. tashhisi
- B. majazi
- C. chuku
- D. nahau

**50.** Maana ya, **kujikuna ajipatapo**, kwa mujibu wa kifungu ni kujitahidi:
- A. kulingana na uwezo wake;
- B. kufuatia shaka aliyo nayo;
- C. kwa kuonyesha ubingwa;
- D. kwa kutaka kujinusuru.